Ripoti ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji kwa Jamii (UUJ)

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke-Dar es Salaam

Februari, 2014

Imeandaliwa na:
Timu ya UUJ-Temeke

SHUKRANI

Kukamilika kwa ripoti hii ni matokeo ya juhudi na kujitoa kwa wadau wanaowakilisha makundi mbalimbali katika jamii ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Timu ya UUJ Manispaa ya Temeke inatoa shukrani za kipekee kwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Temeke, hususan Mheshiwa Sophia Mjema kwa mchango mkubwa alioutoa katika kila hatua kufanikisha kazi hii na hatimaye kukamilika kwa ripoti hii.

Kwa namna ya pekee, Timu ya UUJ ya Manispaa ya Temeke inatoa shukrani za dhati kwa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Temeke chini ya Mstahiki Meya kwa ushirikiano wa dhati katika kuandaa na kuhudhuria mkutano wa waheshimiwa madiwani uliowachagua madiwani wawili (Waheshimiwa Zuhura Dollah na Hamisi Mzuzuri), ambao waliwawakilisha ipasavyo waheshimiwa madiwani katika Timu ya UUJ.

Vilevile, Timu hii inatambua kwa dhati juhudi zilizofanywa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, hususan Mkurugenzi wa Manispaa ndugu Protidas Kagimbo, Mganga Mkuu wa Manispaa Silvia Mamkwe ambao kwa pamoja waliiwezesha Timu ya UUJ ya manispaa ya Temeke kuendesha zoezi zima la UUJ kwa ushirikiano mkubwa.

Mwisho, tunapenda kuwashukuru wawezeshaji wa zoezi hili; Tusekile Mwambetania, Jackson Sikahanga na Lydia Kamwaga kutoka Sikika na watoa huduma za afya wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha zoezi hili katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Kama Mwenyekiti na Mjumbe wa Timu ya UUJ Temeke, napenda kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wenzangu Hulda Ulomi, Mh. Zuhura Dollah, Mh. Hamisi Mzuzuri, Dr. Mashombo Mkamba, Dunia Othman, Khatibu Msumi, Mwajuma Ramadhani, Said Seleman, Ali Kingwande, Phanuel Magogwa, Amina Nassoro, Severine Kalaki, Lucas Mbosa, Zakaria Jorojig na Fr. Amani Chitemo kwa ushirikiano, uvumulivu na kujituma ili kuhakikisha zoezi linakamilika na kuleta tija katika uboreshaji wa huduma za afya ndani ya Manispaa ya Temeke.

Saidi Mbua

Mwenyekiti - Timu ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji kwa Jamii – Temeke

YALIYOMO

SHUKRANI **2**

ORODHA YA VIFUPISHO **4**

PONGEZI **5**

1. SEHEMU YA KWANZA **6**

1.1. Utangulizi **6**

1.1.1. Huduma ya Afya katika Manispaa ya Temeke 7

1.1.2. Vyanzo vya Mapato /Bajeti ya Afya 7

1.1.3. Dawa na Vifaa Tiba 8

1.1.4. Rasilimali Watu 8

1.1.5. VVU na UKIMWI 8

2. SEHEMU YA PILI **9**

2.1. Mchakato wa Zoezi la Ufuatiliaji wa Uwajibikaji kwa Jamii **9**

2.1.1. Uchaguzi wa Wajumbe wa Timu ya UUJ-Temeke 9

2.1.2. Mafunzo kwa Timu ya UUJ 10

2.1.3. Mipango na Mgawanyo wa Rasilimali 10

2.1.4. Usimamizi wa Matumizi 10

2.1.5. Usimamizi wa Utendaji 10

2.1.6. Usimamizi wa Uadilifu 11

2.1.7. Usimamizi wa Uwajibikaji 11

2.2. Uchambuzi wa Nyaraka **11**

2.3. Mbinu Zilizotumika Kukusanya Taarifa **11**

3. SEHEMU YA TATU **12**

3.1. Hoja Zilizoibuliwa na Timu ya UUJ katika uchambuzi wa nyaraka **12**

3.1.1. Uchambuzi wa Mpango Mkakati. 12

3.1.2. Uchambuzi wa Mpango Kabambe wa Afya wa Wilaya 13

Ofisi ya Mganga Mkuu 13

Hospitali ya Temeke 14

Hospitali ya Vijibweni 15

3.2. Hoja zilizoibuliwa na timu ya UUJ katika Kutembelea Vituo **15**

3.3. Huduma za VVU na UKIMWI **18**

4. MAPENDEKEZO NA HITIMISHO **19**

ORODHA YA VIFUPISHO

BOQ	Bid of Quotes (Makadirio ya Gharama)
CAG	Controller and Auditor General – Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
CCHP	Council Comprehensive Health Plan – Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri
CHF	Community Health Fund – Mfuko wa Afya ya Jamii
CHMT	Council Health Management Team – Kamati ya Usimamizi wa Shughuli za Afya za Wilaya
CTC	Counseling and Testing Centre – Kituo cha Ushauri na Upimaji
ICESCR	International Convention for Eco – Social and Cultural Rights - Mkataba wa Kimataifa juu ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni.
MMAM	Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi
MSD	Medical Store Department – Bohari Kuu ya Dawa ya Taifa
O & OD	Opportunity and Obstacle for Development – Fursa na Vikwazo vya Maendeleo
SAM	Social Accountability Monitoring - (Ufuatiliaji wa Uwajibikaji kwa Jamii)
TACAIDS	Tanzania Commission for AIDS – Tume ya Kudhibiti UKIMWI
TAMISEMI	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TBA	Traditional Birth Attendants – Wakunga wa Jadi
UUJ	Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii
VCT	Voluntary Counseling and Testing – Upimaji wa Hiari na Ushauri nasaa
VVU	Virusi vya UKIMWI
WAVIU	Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI

PONGEZI

Katika kutembelea vituo vya huduma, Timu ya UUJ Temeke ilijionea jinsi huduma za afya zinavyotolewa na michango mbalimbali ya wadau wengine wa afya katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Hivyo basi, kwa kuzingatia umuhimu wa wadau katika sekta ya afya, Timu inawapongeza wafuatao;

i. Taasisi ya CCBRT kwa kusaidia kutoa mafunzo ya lugha za alama kwa watumishi wa afya ili waweze kuwasiliana na wagonjwa viziwi hasa wakati wa kutoa huduma ya mama na mtoto.

ii. Pia, Timu ya UUJ Manispaa ya Temeke inalipongeza shirika la MDH kwa kusaidia manispaa katika kutoa na kuboresha huduma za UKIMWI katika manispaa ya Temeke

iii. Zahanati ya Yombo Vituka na hospitali ya vijibweni kwa kuwa na mbinu mbadala za kupokea na kushughulikia malalamiko mbali na ile ya kutumia masanduku ya maoni tu.

iv. Zahanati ya Mbagala Kizuiani kwa kuweka bango linaloanisha makundi ya watu wanostahili kupata msamaha wa gharama za matibabu.

1. SEHEMU YA KWANZA

1.1. Utangulizi

Dhana ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji kwa Jamii (UUJ) inahusu ushiriki wa wananchi katika kufuatilia michakato ya kiutendaji na utoaji huduma ndani ya jamii. Lengo ni kuona kama huduma itolewayo inaleta tija na inazingatia mahitaji halisi ya wananchi. Dhana hii inatoa nafasi kwa wananchi kuwa na uwezo wa kufuatilia mchakato mzima wa upangaji na ugawaji wa rasilimali, usimamizi wa matumizi yake, ufanisi wa watendaji, uzingatiaji wa maadili, na usimamizi wa mamlaka.

Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kuboresha upatikanaji wa huduma za afya katika ngazi ya hospitali ya rufaa-Temeke, vituo vya afya na zahanati, bado Halmashauri inakumbana na vikwazo vingi katika jitihada zake za kuboresha huduma za afya katika Manispaa hiyo. Kukosekana kwa uwajibikaji wa jamii au kutotumia ipasavyo fursa za kuwahusisha wananchi katika kusimamia rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya sekta ya afya ni mojawapo tu ya vikwazo hivyo.

Zoezi la UUJ katika Manispaa ya Temeke lililenga katika kuijengea jamii uwezo wa kushiriki katika kupanga, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za afya katika manispaa yao na pia kuimarisha uwajibikaji wa jamii na watoa huduma ili kuboresha utoaji wa huduma bora za afya katika ngazi zote.

Katika kuhakikisha kuwa kazi hii inafanyika kikamilifu, Timu ya UUJ-Temeke ilijengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo maalum kwa muda wa wiki tatu ambayo yaliiwezesha kuchambua ripoti na taarifa mbalimbali za Halmashauri na kisha kufanya uhakiki kwa kutembelea maeneo ya vituo vya kutolea huduma za afya.

Ripoti hii inaelezea jinsi zoezi lilivyofanyika kuanzia uchaguzi wa wajumbe wa UUJ, uchambuzi wa nyaraka, kutembelea vituo vya huduma za afya, jinsi ambavyo hoja ziliibuliwa na majibu ya utawala kuhusiana na hoja hizo. Ripoti pia imeelezea changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa zoezi na mapendekezo ya Timu.

1.1.1. Huduma ya Afya katika Manispaa ya Temeke

Kulingana na Mpango Kabambe wa Afya wa Wilaya (Comprehensive Council Health Plan – CCHP) wa mwaka 2011/12, ambao ulitumika katika kufanya uchambuzi, ulionesha kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ina hospitali 3, kituo kimoja cha afya na zahanati 36.

1.1.2. Vyanzo vya Mapato /Bajeti ya Afya

Kipindi cha mwaka 2011/12, Halmashauri ya Temeke ilipanga kutekeleza shughuli zake za kutoa huduma ya afya kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali

Vyanzo vya mapato		Kiasi
Ruzuku kutoka serikalini		9,794,410,510
		382,561,000
Mfuko wa pamoja		1,597,999.4000
HSDG		401,588,000
Mapato ya ndani ya Halmashauri	Fedha za matumizi ya kawaida	150,000,000
	Fedha za maendeleo	800,000,000
LGDCG	Fedha za maendeleo	800,000,000
Vyanzo visivyo vya kifedha	Madawa na vifaa tiba	496,000,000
Uchangiaji gharama	Malipo ya mtumiaji	741,611,701
Vinginevyo	LHL	90,566,000
JUMLA		15,254,736,611

Chanzo: Temeke CCHP, 2011/12

1.1.3. Dawa na Vifaa Tiba

Bohari kuu ya dawa ndiye msambazaji mkuu wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya kwenye Manispaa ya Temeke. Hospitali ya Temeke hupata wastani wa shilingi milioni 60 na Hospitali ya Vijibweni shilingi milioni 18 kwa ajili ya matumizi ya dawa na vifaa tiba katika kila robo ya mwaka.

Vituo vya afya hupokea wastani wa shilingi milioni 2.3 na zahanati shilingi milioni 1.05 kwa kila robo mwaka kwa ajili ya matumizi ya dawa na vifaa tiba kwa kutumia mfumo wa (Integrated Logistics System – ILS). Mfumo huu huruhusu Vituo vya Afya na Zahanati kuagiza dawa kutoka MSD kulingana na mahitaji yao.

1.1.4. Rasilimali Watu

Kwa kipindi cha 2011, Manispaa ya Temeke ilikuwa na jumla ya watumishi wa afya 1279 ambao waligawanyika katika hospitali, vituo vya afya na zahanati. Kiasi hiki cha watumishi wa afya bado hakitoshelezi ikilinganishwa na mahitaji ambapo kwa sasa kuna upungufu wa watumishi 644 sawa na asilimia 50.4%.

1.1.5. VVU na UKIMWI

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ina vituo 13 vya kutolea huduma za VVU na UKIMWI. Programu za UKIMWI zinaendeshwa kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi za Tiba Muhimbili pamoja na Chuo Kikuu cha Havard. Idadi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa mwaka wa 2010/11 ilikuwa 22,861.

2. SEHEMU YA PILI

2.1. Mchakato wa Zoezi la Ufuatiliaji wa Uwajibikaji kwa Jamii

Ili kufanya zoezi la UUJ kuwa shirikishi na linalomilikiwa na jamii, Sikika iliratibu zoezi hili katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza, Sikika ilifanya mikutano na wadau wa afya iliyolenga kuelezea umuhimu wa zoezi hili na namna litakavyofanyika, na pia kuchagua wajumbe wa timu ya UUJ kutoka katika makundi mbalimbali ya kijamii.

Sehemu ya pili, ilikuwa ni kuzungumza na wataalam (CHMT/CMT) ili kupata ufafanuzi wa masuala mbalimbali yaliyoibuliwa wakati wa uchambuzi wa nyaraka za Halmashauri na baada ya kutembelea vituo vya kutolea huduma za afya. Mkutano huu, ulifuatiwa na mkutano wa wadau wa afya ambao pia ulilenga kuwasilisha rasimu ya ripoti ya UUJ kwa wadau wa afya ili nao wapate fursa ya kuijadili na kutoa mapendekezo ya pamoja ya kuboresha huduma za afya ndani ya Manispaa ya Temeke.

2.1.1. Uchaguzi wa Wajumbe wa Timu ya UUJ-Temeke

Kwa Manispaa ya Temeke Timu iliundwa na wajumbe 16. Uwakilishi wao ulitokana na makundi yafuatayo: wananchi, madiwani, asasi za kiraia, Kamati ya Kudhibiti UKIMWI ya Wilaya, kamati za vituo vya kutolea huduma za afya, Bodi ya Afya ya Wilaya, uwakilishi wa CMT, kundi la viongozi wa dini, uwakilishi wa watu wenye mahitaji maalumu (walemavu) na watendaji wa kata.

Zoezi la uundaji wa Timu za UUJ, lilianzia katika ngazi ya jamii kwa kupata uwakilishi wa wananchi kupitia mikutano ya kijamii ambapo wananchi walichaguliwa kwa kupigiwa kura ya siri katika mikutano ya jamii iliyofanyika ndani ya kata zao, wakati waheshimiwa madiwani walichaguliwa katika mkutano wa Baraza Kuu la Madiwani wa Halmashauri. Uwakilishi wa makundi mengine ya kijamii ulipitia mkutano mkuu wa wadau, ambapo wajumbe wa kila kundi waliteua mwakilishi wao. Baada ya uteuzi huo, jumla ya wawakilishi 16 kutoka kila kundi waliungana na kutambulishwa mbele ya wajumbe wa mkutano wa wadau wa afya kama Timu ya UUJ Manispaa ya Temeke ambayo imefanya kazi kwa niaba ya wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Baada ya kuundwa, Timu hii ilichagua Mwenyekiti wao ambaye ni mjumbe wa Bodi ya Afya ya Wilayai, ndugu

Saidi Mbua na Afisa Mtendaji wa Kata ya Chang'ombe, Bi. Hulda J. Ulomi alichaguliwa kuwa Katibu wa Timu hiyo.

2.1.2. Mafunzo kwa Timu ya UUJ

Timu ya UUJ ilipatiwa mafunzo sambamba na kufanya uchambuzi wa nyaraka kwa vitendo kwa kipindi cha wiki tatu. Mafunzo hayo yaliyotolewa chini ya uratibu wa Sikika yaliiwezesha Timu kuelewa masuala mbalimbali yahusuyo Halmashauri na sekta ya afya na UKIMWI kwa ujumla. Uelewa wa washiriki ulifanikisha zoezi la uchambuzi wa nyaraka ambao ulifanywa kwa umakini mkubwa. Wajumbe wa Timu walipata fursa ya kufafanuliwa kwa kina hatua tano za UUJ, umuhimu na nyenzo zinazostahili kutumika katika kila hatua. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:

2.1.3. Mipango na Mgawanyo wa Rasilimali

Timu ilipatiwa mafunzo kuhusu mipango na mgawanyo wa rasilimali. Wajumbe walijifunza namna mipango inavyopaswa kuandaliwa kwa kuhusisha jamii na kuzingatia vipaumbele vya jamii. Katika mafunzo haya Timu ilijifunza mambo yafuatayo: nini maana ya mpango mkakati; misingi ya mpango mkakati, namna ya kuibua vipaumbele vya jamii kwa pamoja; na ushiriki wa jamii katika kuandaa mipango.

Aidha timu ilishiriki katika uchambuzi wa mpango mkakati na mpango kabambe wa afya na mipango ya UKIMWI.

2.1.4. Usimamizi wa Matumizi

Katika hatua hii, Timu ilijifunza maana ya Usimamizi wa Matumizi; umuhimu wa kusimamia matumizi; usimamizi wa matumizi na uwajibikaji kwa jamii; mambo ya kuangalia kwenye ripoti za utekelezaji wa shughuli za afya na UKIMWI pamoja na taarifa za mifumo ya usimamizi wa fedha na ukaguzi wa ndani.

2.1.5. Usimamizi wa Utendaji

Timu ilipatiwa mafunzo ya namna utendaji unavyopaswa kusimamiwa na vyombo vya usimamizi vilivyopo katika ngazi mbalimbali serikalini. Pia wananchi walijifunza wajibu wao katika kusimamia utendaji katika ngazi ya jamii ili kufanikisha upatikanaji na utoaji wa huduma bora za afya.

2.1.6. Usimamizi wa Uadilifu

Hatua hii ilitoa fursa kwa Timu ya UUJ kujifunza maana ya Usimamizi wa Uadilifu kwa Jamii; kanuni na sheria katika Usimamizi wa Uadilifu; Usimamizi wa Uadilifu kwa Umma kwa mtazamo wa Haki za Msingi za Binadamu. Pia, Timu ilijifunza namna ya kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi/ usahihi pamoja na kuhakikisha kuwa utaratibu wa maamuzi unakuwa wazi kwa umma kiasi cha kuruhusu wananchi kuhoji na kufanya marekebisho.

2.1.7. Usimamizi wa Uwajibikaji

Katika hatua hii ya tano, timu ilipatiwa mafunzo juu ya maana ya uwajibikaji, umuhimu wa kufuatilia uwajibikaji, vyombo vya usimamizi wa uangalizi na mahitaji muhimu ya uangalizi wa uwajibikaji. Timu pia ilijifunza namna watendaji wakuu wa serikali wanavyopaswa kuwajibika dhidi ya kanuni za ufanisi, uaminifu na unyoofu katika utendaji kazi wao.

2.2. Uchambuzi wa Nyaraka

Kama chombo cha usimamizi/ufuatiliaji, Timu ya UUJ ya manispaa ya Temeke ilifanya mapitio ya nyaraka zifuatazo:-

- Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke 2010/11-2012/13
- Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri a 2011/12
- Mihtasari ya vikao vya Baraza la Madiwani 2011/12
- Mihtasari ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI ya Wilaya 2011/12
- Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi (Kamati ya UKIMWI)
- Ripoti za Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Halmashauri

2.3. Mbinu Zilizotumika Kukusanya Taarifa

Kwa kutumia dodoso lililoandaliwa kutokana na taarifa za uchambuzi wa nyaraka, Timu ya UUJ ilikusanya taarifa juu ya hatua mbalimbali zilizofikiwa katika miradi na hali halisi za utoaji wa huduma katika vituo ikiwemo uwepo na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, idadi ya watumishi waliopo vituoni kulingana na mahitaji, nyumba za watumishi wa afya, huduma za VVU na UKIMWI na upatikanaji wa huduma kwa watu walio na ulemavu, hasa viziwi. Vilevile, Timu ilihoji juu ya upatikanaji wa taarifa za fedha, mchakato wa uandaaji wa bajeti za vituo na ushirikiano baina ya kituo, kata, waheshimiwa madiwani, kamati ya usimamizi wa kituo husika pamoja na halmashauri. Timu pia ilitaka kujua kama zipo na utendaji kazi wa kamati za kudhibiti UKIMWI katika ofisi za kijiji pamoja na ofisi za kata husika.

3. SEHEMU YA TATU

3.1. Hoja Zilizoibuliwa na Timu ya UUJ katika uchambuzi wa nyaraka

3.1.1. Uchambuzi wa Mpango Mkakati.

Mpango mkakati ni hatua muhimu katika kufikia mipango ya mwaka; mgawanyo sahihi wa rasilimali, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa utendaji, usimamizi wa uadalifu na usimamizi wa uwajibikaji. Utendaji na utekelezaji bora wa mpango mkakati huchangia utambuzi wa haki za binadamu na huduma bora za jamii; hivyo mpango mkakati ni lazima uwe na dira, dhamira na malengo.

Ili kufikia malengo lazima kuwe na shughuli zilizotengewa fedha/bajeti ili kuzitekeleza. Vilevile, mpango mkakati unapaswa kuwa na viashiria vinavyopimika, mchakato wa ufuatiliaji na tathmini kuangalia iwapo kama malengo yamefikiwa. Kama hayajafanikiwa ni lazima mpango uainishe changamoto katika utekelezaji wake na kueleza nini kifanyike kukabiliana nazo. Zaidi ya hayo, mpango mkakati lazima uzingatie mahitaji ya jamii na kuyapa kipaumbele.

Ushirikishaji wa jamii ni kipengele muhimu katika maandalizi ya mpango mkakati. Hivyo basi, mpango mkakati unatakiwa kuwa wazi, wenye uwajibikaji na shirikishi kwa wanajamii husika ili kuwawezesha wanajamii kudai ufafanuzi, uthibitisho na uhalalisho wa chochote kilichopangwa kufanyika kupitia mpango mkakati.

Mpango mkakati mzuri, hutoa mwongozo wa shughuli ambazo zitafanyika, gharama zake na muda wa utekelezaji wake. Mpango Mkakati pia, huimarisha usimamizi wa ndani pamoja na usimamizi wa nje wa matumizi na huziwezesha halmashauri kusimamia utendaji dhidi ya mipango yake.

Mpango mkakati wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ulianza kutekelezwa mwaka 2010 na huandaliwa upya kila baada ya miaka mitatu. Timu ya UUJ ilibaini na kuridhia kuwa Mpango Mkakati wa Wilaya ya Temeke umeonesha dira, dhamira na Malengo makuu.

Mpango mkakati huo una uchambuzi wa kina na umeonesha mazingira ya nje na ndani, mikataba ya kimataifa na kitaifa, na umezingatia dira na sera za taifa.

Hoja za Timu Kuhusu Mpango Mkakati

Hoja ya Timu: Timu ilibaini kuwa lugha iliyotumika kuandaa mpango mkakati ni Kiingereza ambayo si lugha rafiki kwa wananchi wote wa Manispaa ya Temeke. Hivyo, Timu ilitaka kujua kama Manisapaa ina nakala za Kiswahili za Mpango Mkakati ili kutoa fursa kwa wananchi wote kuusoma.

Majibu ya utawala: Taarifa za Mpango Mkakati na Mpango Kabambe wa Afya wa Wilaya zipo katika lugha za Kiswahili na Kiingereza.

Ushauri wa Timu: Nakala za Kiswahili ziwe zinatolewa kwa wadau wa maendeleo pale zinapohitajika.

Hoja ya Timu: Mpango Mkakati umeelezea mafanikio yaliyofikiwa na Halmashauri, lakini haukuonesha wazi rasilimali/fedha zitakazotumika kutekeleza mpango mkakati huu. Timu ilitaka kujua kwa nini hakuna uchambuzi wa kina juu ya uwezo wa rasilimali fedha wa Manispaa.

Majibu ya Utawala: Mpango mkakati sio lazima uwe na bajeti.

3.1.2. Uchambuzi wa Mpango Kabambe wa Afya wa Wilaya

Ofisi ya Mganga Mkuu

Katika shughuli **Na. 1.7.4.2,** mpango wa afya wa Halmashauri unaonesha Idara ya Afya ilipanga kuwawezesha wafanyakazi 80 kutekeleza majukumu yao kwa Tsh. 31,400,000/-. Ripoti ya utekelezaji ya mwaka 2012/13 inaonesha kazi hii haikutekelezwa kutokana na kutokutengewa fedha. **Hoja ya Timu:** Timu ilitaka kupata ufafanuzi kama kuna utaratibu wowote uliwekwa wa kuwawezesha watumishi kupata mafunzo hayo ili waweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyokuwa imepangwa?

Majibu ya Utawala: Vyanzo vingine vilitumika kuwawezesha watumishi japo havikuoneshwa kwenye ripoti

Shughuli **Na. 1.8.8.1** Idara ilipanga kufanya ukarabati wa majengo kwa Tsh. 6,600,000/- ifikapo mwaka 2012. Katika ripoti ya utekelezaji, kazi hii ilionekana imetekelezwa kwa 100%. Vyumba 6 vilipakwa rangi na kubadilishwa dari. Kazi hii imejirudia kwa namba tajwa hapo juu (1.8.8.1) ikiwa imetengewa kiasi cha Tsh.3,000,000/-.

Hoja ya Timu: Timu ilitaka kujua, kwa nini kazi hii ilijirudia mara mbili ikitumia namba moja (1.8.8.1) na gharama tofauti?

Majibu ya Utawala: Kazi hii ilikuwa na vyanzo viwili vya fedha.

Hospitali ya Temeke

Kazi **Na. 2.1.7.15** Idara kupitia Hospitali ya Temeke ilipanga kutengeneza magari 3 kwa Tsh. 4,927,153. Ripoti ya utekelezaji inaonesha kazi hiyo ilitekelezwa kwa 100%; lakini haijaainisha aina na namba za magari yaliyotengenezwa.

Hoja ya Timu: Katika kazi hii Timu ilitaka kujua kama kazi ilifanyika na ni magari gani yalitengenezwa, kutokana na kukosekana kwa aina na namba za magari?

Majibu ya Utawala: Ni kweli magari yalitengenezwa, mapungufu ni kutotajwa kwa aina au namba za magari. Utawala utafanyia kazi suala hili.

Kazi **Na 2.8.1.3** Idara ilipanga kuhakikisha magari 4 na mashine 1 katika hospitali ya Temeke yanakuwa katika hali nzuri kwa Tsh 22, 000,000/-. Kazi hii ilitekelezwa kwa Tsh.10, 938,500/-

Hoja ya Timu: Japo kazi inaonekana kufanyika, lakini ripoti haikuainisha ni magari gani yaliyotengenezwa na mashine zipi zilizotengenezwa. Pia Bakaa ya fedha hizi haikutajwa.

Majibu Utawala: Ni kweli magari yalitengenezwa, mapungufu ni kutotajwa kwa aina

au namba za magari pamoja na mashine zilizotengenezwa.

Hospitali ya Vijibweni

Kazi **Na.3.8.3.7** Idara ilipanga kufanya matengenezo ya gari na mashine kwa Tsh. 9,280,000 na zikatumika zote. Mpango haukuainisha magari mangapi yatatengenezwa japo magari 4 yalitengenezwa. **Hoja ya Timu:** Timu haikuweza kujua ni magari gani wala aina gani ya mashine zilizotengenezwa kwa kipindi hicho, hata hivyo mashine zilizotengenezwa hazikuonekana katika ripoti ya utekelezaji.

Majibu ya Utawala: Kwa mwaka gari inatengenezwa zaidi ya mara moja, jenereta pia iliharibika ikatengenezwa zaidi ya mara mmoja. Changamoto iliyopo ni kuwa taarifa hizi hazipo kwenye ripoti ya utekelezaji.

3.2. Hoja zilizoibuliwa na timu ya UUJ katika Kutembelea Vituo

Baada ya uchambuzi wa nyaraka mbalimbali za afya na UKIMWI, Timu ya UUJ iliainisha masuala na miradi mbalimbali iliyohitaji kuhakikiwa katika vituo vya huduma kulingana na uchambuzi na tathmini ya taarifa zilizopitiwa. Lengo la ziara hii ilikuwa ni kulinganisha taarifa za utekelezaji na hali halisi, kuhakiki miradi inayotekelezwa na serikali kupitia Halmashauri. Jumla ya vituo 22 vya huduma za afya (hospitali 3, vituo vya afya 2, zahanati 17) vilivyopo ndani ya Manispaa ya Temeke vilitembelewa

Hali halisi baada ya kutembelea vituo vya kutolea huduma za afya	**Ufafanuzi kutoka utawala**
Timu ilibaini kuwepo kwa mawasiliano hafifu kati ya uongozi wa kata na watoa huduma za afya, pia baadhi ya kamati za afya hazitembelei vituo hivyo kabisa.	Tatizo lipo pande zote mbili (Vituo na Kata)**,** hivyo pande zote zijiweke sawa ili kuboresha mahusiano hayo. Utambulisho wa watumishi wapya utafanyika kwa pande zote mbili.
Posho za malipo ya saa z**a ziada hazilipwi kwa wakati (huchukua kati ya miezi 3 hadi 6), hii inapunguza morali ya kazi.**	Posho zinalipwa lakini siyo kwa wakati hasa kwa vile vituo vyenye mapato kidogo. Na vituo vingine vyenye mapato

	makubwa huchelewa kutokana na baadhi ya waganga wafawidhi kutokuwasilisha taarifa kwa wakati.
Imeonekana kuna u**salama mdogo kwenye vituo kutokana na ulinzi hafifu. Mfano**, **vituo vya Mbande, Yombo Vituka havina uzio**.	Suala hili lilichukuliwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi.
Timu pia ilibaini baadhi ya watumishi wa afya hawakai katika nyumba walizopewa katika vituo.	Utawala ulieleza kutambua kuwepo kwa tatizo hilo na kusema linashughulikiwa ili kupata utatuzi
Katika ziara hii ilibanika kuwa: - ▪ **Baadhi ya vituo vinauza kadi za akina mama na watoto** kwa **TSh.1,000-1500,** ▪ **Uuzwaji wa dawa za wajawazito (madini, damu),** ▪ **Huduma za uzazi wa mpango zinalipiwa katika baadhi ya vituo vya huduma**, ▪ **Baadhi ya vituo vinatoza watoto chini ya miaka mitano**.	Utawala ulishauri mambo yafuatayo: - ▪ Kutokana na suala hili kujulikana, kamati za afya ziliaswa kulisimamia ipasavyo na kuhakikisha wanamaliza suala hili. ▪ Pia wahusika watakaobainika wachukuliwe hatua za kinidhamu ▪ Wananchi waelimishwe haki zao na watoe taarifa kwa wahusika
Baadhi ya vituo havina miundombinu rafiki kwa walemavu na wazee (Mfano, **Mbagala Rangitatu, Mwongozo**)	Hadi sasa wameboresha tofauti na zamani vimebaki vichache ambavyo vitafanyiwa kazi
Wengi wa watoa huduma za afya hawajapata mafunzo ya lugha ya alama ili kuwawezesha kuwasiliana na viziwi wakati wa kutoa huduma za afya	Suala la lugha ya alama lilichukuliwa ili kufanyiwa kazi
Kuna tatizo la usafiri wa dharura katika maeneo ya	Suala la magari ya wagonjwa

nje ya mji, hivyo utawala uangalie suala hili	(ambulance) linashughulikiwa; (2013, ambulance 3 zimenunuliwa)
Kuna tatizo la maji katika vituo vya Amani, **Gomvu na Mjimwema**	Maji ya Amani, Gomvu ni ya chumvi hivyo mabomba huchakaa haraka, lakini mhandisi ataelezwa ili abadilishe
Baadhi ya vituo havina mifumo ya kutolea maoni/malalamiko. Vituo vingi havina mbao za matangazo hivyo:- **- Taarifa zinabandikwa ukutani** **- Vituo vingine** taarifa **hazibandikwi kabisa**	Suala la sanduku la maoni; ni changamoto ambayo imekuwa ikiongelewa mara kwa mara lakini tunalichukua tutalifanyia kazi. - Suala la mbao za matangazo litafuatiliwa
Ushiriki mdogo **wa wananchi katika kamati na bodi za afya, mfano kituo cha Mbagala Kizuaini**	Utawala hawakutoa ufafanuzi wowote kuhusiana na suala hili.
Timu pia ilibaini wodi za wazazi zinakosa faragha **mfano**, **Tambukareli, Majimatitu hakuna uzio**	Majimatitu wapo kwenye mchakato wa kujenga uzio
Kuna m**azingira hatarishi kiafya kutokana na kuwepo kwa mfereji wa majitaka ndani ya hospitali ya Temeke**	Mfereji wa maji machafu hospitali ya Temeke ni suala ambalo linahitaji majadiliano na wadau wengine. kwa sababu ni suala la siku nyingi

3.3. Huduma za VVU na UKIMWI

Baada ya kutembelea vituo vya kutolea huduma za afya timu ilibaini mambo yafuatayo:-

- Baadhi ya vituo havikuwa na vyumba vya kutolea ushauri nasaha (Zahanati) mfano Pemba Mnazi,
- Kamati za UKIMWI zipo lakini hazikutani wala hazifanyi kazi,
- Utekelezaji wa shughuli ambazo hazipo kwenye mpango katika ripoti ya utekelezaji (2011/12) ajenda namba 3 uk. wa tano, Timu ilibaini kuwa kuna baadhi ya kazi zilifanyika pasipo kuwepo kwenye mpango kazi,
- Asilimia kubwa ya shughuli za UKIMWI hutegemea fedha za wafadhili, hivyo Timu inashauri Halmashauri ibuni vyanzo vya ndani ili iweze kushughulikia matatizo ya UKIMWI bila kuwa tegemezi kwa kiasi kikubwa.

4. MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

Baada ya kupitia nyaraka mbalimbali na kutembelea vituo vya huduma za afya, Timu iliridhishwa na miundo na uzingatiaji wa miongozo ya uandaaji wa nyaraka hizo. Baadhi ya masuala ambayo Timu inashauri kufanyiwa marekebisho katika nyaraka ni pamoja na uainishaji wa taarifa kwa kina, kutumika kwa lugha rahisi ya Kiswahili, kufanyika kwa tathmini ya kina na upembuzi yakinifu wa mahitaji ya wananchi. Pia Timu inashauri kuwa Halmashauri iongeze ushiriki wa wananchi wakati wa uandaaji wa mipango na wakati wa utekelezaji wake.

Kutokana na matokeo ya zoezi zima la UUJ katika Manispaa ya Temeke, Timu ya UUJ inapendekeza yafuatayo;

- Miundombinu kwa watu wenye ulemavu na wazee iboreshwe.
- Mahusiano kati ya vituo vya huduma ya afya na ofisi za kata yaboreshwe kwa maana ya watendaji wa kata kutembelea vituo vya huduma mara kwa mara.
- Siku ya UKIMWI duniani iadhimishwe kitaifa, wilaya hadi kata ili kutoa fursa Kwa wananchi wote kupata elimu juu ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI.
- Taarifa za mapato na matumizi ya vituo vya huduma zibandikwe katika mbao za matangazo.
- Mafunzo ya lugha ya alama yatolewe kwa watoa huduma waliopo na yaingizwe katika mitaala ya elimu ya watoa huduma.
- Manispaa ichangie shughuli za ulinzi na kutoa miongozo ya kima cha chini cha mishahara kwa walinzi wa vituo vya huduma ili kuepuka wizi unaoweza kujitokeza kutokana na mishahara midogo wanayolipwa walinzi hao kwa sasa na kupelekea kuacha kazi zao.

Kazi ya ufuatiliaji wa uwajibikaji kwa jamii iliyotekelezwa na Timu ya UUJ imeibua hoja mbalimbali ambazo tunaamini ni chachu ya mabadiliko kwa Halmashauri ya Wilaya ya Temeke, hususan Idara ya Afya. Katika utekelezaji wa kazi hii, Timu ilikutana na changamoto mbalimbali. Timu inaamini kuwa mchakato huu wa ufuatiliaji uwajibikaji kwa jamii una manufaa makubwa kwa jamii na Halmashauri kwa ujumla, kwani pamoja na kutoa mafunzo maalum, umeonesha uwezo na changamoto inazopata Halmashauri, kitu ambacho ni

msaada mkubwa katika kuleta mabadiliko, hususan kwenye Idara ya Afya na utoaji wa huduma za afya kwa ujumla.

Ni imani kubwa ya Timu hii kuwa, ili Manispaa iweze kuwajibika ipasavyo kwa jamii, ni wazi kuwa kazi kama hii ni muhimu kufanyika kwa idara zote mara kwa mara. Hivyo basi, kwa imani hiyo, Timu inashauri Manispaa ishirikiane na Sikika na wadau wengine ili kuiwezesha Timu hii iwe endelevu na iweze kufuatilia uwajibikaji kwa jamii katika idara nyingine zote za Halmashari ili kufikia haki za binadamu na kukidhi mahitaji ya jamii.